KATIBA YA CHAMA CHA KIKOMINISTI CHA CHINA

KATIBA YA CHAMA CHA KIKOMINISTI CHA CHINA

Imepasishwa Katika Mkutano Mkuu
wa Tisa wa Kitaifa wa Wajumbe
wa Chama cha
Kikoministi cha China,
Aprili 14, 1969

OFISI YA UCHAPAJI WA LUGHA ZA KIGENI
PEKING 1969

Uchapaji wa Mwanzo
Kitabu cha Mfukoni 1969

Kimepigwa chapa katika Jamhuri ya Watu wa China

MLANGO WA KWANZA

PROGRAMU KUU

Chama cha Kikoministi cha China ni chama cha kisiasa cha tabaka la kifanya kazi.

Programu ya msingi ya Chama cha Kikoministi cha China ni kulipindua kabisa tabaka la kibepari na matabaka yote ya kinyonyaji da-

mu, kufanya udikteta wa tabaka la kifanya kazi kuchukua mahala pa udikteta wa tabaka la kibepari na kufanya usoshalisti kuushinda ubepari. Madhumuni ya mwisho kabisa ya Chama ni kutimiza Ukominisiti.

Chama cha Kikominisiti cha China ni oganezeshen ya watangulizi yenye ujana na hamasa kubwa, ambayo yamewakusanya watu walioendelea mbele wa tabaka la kifanya kazi, na kuongoza

tabaka la kifanya kazi na umma wa kimapinduzi katika kupigana na adui wa kitabaka.

Chama cha Kikoministi cha China kinafanya Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung kuwa ni msingi wa nadharia wa kuongoza fikra zake. Fikra Mao Tsetung ni Umarx-lenin katika zama ambayo ubeberu unaendea kubomoka kwa pande zote, na usoshalisti unasonga mbe-

le kuendea ushindi duniani kote.

Tokea nusu karne iliyopita, katika kuyaongoza mapigano makubwa ya China kutimiza mapinduzi ya udemokrasi mpya, katika kuyaongoza mapigano makubwa ya mapinduzi ya kisoshalisti na ya ujenzi wa kisoshalisti wa China, katika mapigano makubwa ya zama tuliyo nayo ya vugu vugu la kikoministi la kilimwengu ya kupinga ubeberu, urivishe-

nisti wa kisasa na wapinga maendeleo wa nchi mbali mbali, Komredi Mao Tsetung ameunganisha ukweli unaofaa popote wa Umarx-lenin na matendo hasa ya mapinduzi, ameurithi, ameuhami na ameukuza Umarx-lenin, na ameuinua juu Umarx-lenin kufikilia daraja mpya kabisa.

Komredi Lin Piao siku zote ananyanyua juu bendera kubwa nyekundu ya Fikra Mao Tsetung, na

ameutekeleza na kuuhami kwa imani kubwa kabisa na kwa uthabiti kabisa msimamo wa kimapinduzi wa tabaka la kifanya kazi wa Komredi Mao Tsetung. Komredi Lin Piao ni komredi mkubwa wa kimapigano wa Komredi Mao Tsetung na ni mrithi wake.

Chama cha Kikoministi cha China — Komredi Mao Tsetung akiwa ni Kiongozi wake — ni Chama kikuu, kitukufu na sahihi, na ni

kiini cha uongozi cha watu wa China. Baada ya majaribio marefu ya mapigano ya kitabaka ya kunyakua na kuimarisha hatamu za kiserikali kwa silaha, Chama kimeimarika na kukua katika mapigano ya kupinga misimamo ya uopotyunisti wa Kulia na wa "Kushoto", na kikiwa na moyo mkubwa kinasonga mbele kwa ushujaa kwenye njia ya mapinduzi ya kisoshalisti na ya ujenzi wa kisoshalisti.

Jamii ya kisoshalisti ni kipindi kirefu cha kutosha cha kihistoria. Katika kipindi hichi cha kihistoria, tokea mwanzo hadi mwisho, yapo matabaka, hitilafu za kitabaka na mapigano ya kitabaka, yapo mapigano ya njia mbili baina ya usoshalisti na ubepari, ipo hatari ya kurudishwa kwa ubepari, na yapo matisho ya upinduzi na ushambulizi kutokana na ubeberu na urivishenisti wa kisasa. Hitilafu hizi haziwezi kutanzuliwa ila kwa kutegemea nadharia ya Umarx ya kuendelea na mapinduzi na matendo yaliyoongozwa na nadharia hiyo. Mapinduzi Makubwa ya Utamaduni ya Tabaka la Kifanya Kazi ya nchi yetu, ndiyo mapinduzi makubwa ya kisiasa ya kupinga tabaka la kibepari na matabaka yote ya kinyonyaji damu yanayofanywa na tabaka la kifanya kazi chini ya hali ya kisoshalisti.

Chama kizima lazima kinyanyue juu bendera kubwa nyekundu ya Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung, kiwaongoze mamia ya mamilioni ya watu wa makabila mbali mbali wa nchi nzima kuendelea kufanya mavugu vugu makubwa matatu ya kimapinduzi — mapigano ya kitabaka, mapigano ya utoaji vitu na mazao, na majaribio ya kisayansi — kiimarishe na kutilia nguvu udikteta wa tabaka la kifanya kazi,

kifuate kanuni ya kujiendesha kwa nguvu zetu wenyewe na kujistawisha kwa kujitegemea wenyewe na kufanya jihadi kwa ushupavu, kutumia nguvu zote na kupigania kutangulia mbele katika kujenga usoshalisti kwa wingi zaidi, mbio zaidi, ubora zaidi na kwa gharama ndogo zaidi.

Chama cha Kikoministi cha China kinashikilia udugu wa kilimwengu wa tabaka la kifanya kazi, kinaun-

gana kwa uthabiti pamoja na vyama vya kisiasa na vikundi vya Umarx-lenin hasa katika dunia nzima, kinaungana pamoja na tabaka la kifanya kazi, watu wanaokandamizwa na mataifa yanayokandamizwa katika dunia nzima, kupigania kwa pamoja kuangamiza ubeberu ukiongozwa na Marekani, kuangamiza urivishenisti wa kisasa ambao kiini chake kikiwa ni ki-

kundi cha wahaini warivishenisti cha Kisoviet, na kuwaangamiza wapinga maendeleo wa nchi mbali mbali na kuangamiza mpango wa kunyonya damu binadamu kwa binadamu katika dunia, ili binadamu wote wapate ukombozi.

Wanachama wa Chama cha Kikoministi cha China ambao wameazimia kidete maisha kupigania Ukoministi, lazima watie nia imara,

wasiogope kujitolea mhanga, wazishinde shida zote ili wajipatie ushindi!

MLANGO WA PILI

UWANACHAMA

Kifungu cha Kwanza: Kila mfanya kazi, mkulima masikini, mkulima wa kati wa daraja ya chini, mwana-jeshi wa kimapinduzi na mwana-mapinduzi mwen-gineo wa China aliyetimia umri wa miaka 18, anaweza kuwa mwanachama wa Cha-

ma cha Kikoministi cha China akiikubali Katiba ya Chama, kuingia katika oganezeshen ya Chama na kufanya kazi kwa bidii humo ndani, kutekeleza maazimio ya Chama, kufuata nidhamu ya Chama na kulipa ada za Chama.

Kifungu cha Pili: Wanaotoa maombi ya kuingia katika Chama lazima mmoja mmoja atekeleze mambo yanayotakikana ya kuingia katika Chama, ajulishwe

kwenye Chama na wanachama wawili, ajaze fomu ya maombi ya kuingia katika Chama, akaguliwe na tawi la Chama, ambalo lazima liyasikilize kwa mapana na marefu maoni ya umma walio ndani na nje ya Chama, akubaliwe katika mkutano wa tawi na atolewe idhini na kamiti ya Chama inayoongoza tawi hilo.

Kifungu cha Tatu: Wanachama wa Chama cha Kikoministi cha China lazima

watekeleze mambo yafuatayo:

1) Kusoma na kutumia vitendoni Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung;

2) Kupigania maslaha ya sehemu kubwa ya watu wa China na dunia;

3) Kuweza kuungana na sehemu kubwa ya watu, wakiwemo wale ambao walifanya makosa katika kuwapinga wao na baadae wanajitahidi katika kusahihisha makosa yao. Lakini,

lazima kujihadhari hasa na wale wanaojijenga, wapikao majungu na wenye nyuso mbili, na kuzuia watu wabaya kama hao wasije wakanyakua uongozi wa Chama na wa taifa katika daraja mbali mbali na kuhakikisha hatamu za uongozi wa Chama na wa taifa daima ziwe mikononi mwa wana-mapinduzi wa Kimarx;

4) Kushauriana na umma pakiwepo jambo; na

5) Kuthubutu kutoa makosa na kujitoa makosa.

Kifungu cha Nne: Wanachama wakiharibu nidhamu ya Chama, kwa mujibu wa madaraka na mamlaka yake, oganezeshen za Chama katika daraja mbali mbali zawapa adabu ya onyo, au ya onyo kali, au ya kuwatoa kwenye cheo ndani ya Chama, au ya kubakizwa katika Chama ili kujaribiwa, au ya kufukuzwa kutoka katika

Chama, kwa kutegemea hali ilivyo.

Kwa mwanachama, muda mrefu kabisa wa kubakizwa katika Chama ili kujaribiwa usipindukie miaka miwili. Mnamo muda huo, yeye hana haki ya kutoa uamuzi, ya kuchagua wala ya kuchaguliwa.

Mwanachama aliyepotewa kabisa na moyo wa kimapinduzi, ambaye hatengenei hata baada ya kuelimishwa, inampasa atoke

katika Chama kwa kuelezwa.

Mwanachama akidai kutoka katika Chama, jina lake lifutwe kwa kupasishwa katika mkutano wa tawi, na kutoa ripoti kwa kamiti ya Chama inayoongoza tawi hilo kufanya kumbu kumbu. Ikihitajika, jambo hilo litangazwe hadharani miongoni mwa umma walio nje ya Chama.

Wale waliothibitika kuwa mahaini, majasusi, wachukua njia ya kibepari wenye mamlaka ambao hawakubali kuongoka mpaka kufa kwao, wapotovu na wale wa matabaka yenye uhasama nasi waliojipenyeza ndani ya Chama lazima wafukuzwe katika Chama na asilan wasiruhusiwe tena kuingia katika Chama.

KANUNI YA OGANEZESHEN YA CHAMA

Kifungu cha Tano: Kanuni ya oganezeshen ya Chama ni demokrasi-uongozi.

Maidara ya uongozi ya Chama katika daraja mbali mbali yachaguliwa kwa njia

ya mashauriano ya kidemokrasi.

Chama kizima lazima kifuate nidhamu ya namna moja, yaani mtu binafsi afuate oganezeshen ya Chama, wachache wawafuate walio wengi, daraja ya chini ifuate daraja ya juu na Chama kizima kiifuate Kamiti Kuu.

Maidara ya uongozi ya Chama katika daraja mbali mbali yanapaswa, kwa muda

uliowekwa, kutoa ripoti ya kazi kwa mkutano mkuu wa wajumbe au mkutano wa wanachama, siku zote kusikiliza maoni ya umma walio ndani na nje ya Chama na kukubali usimamizi wao. Wanachama wanayo haki ya kutoa makosa na mashauri kwa oganezeshen za Chama na wakuu wao katika daraja mbali mbali. Ikiwa mwanachama fulani anayo maoni tofauti kuhusu maa-

zimio au maelekezo ya oganezeshen ya Chama, anaruhusiwa kuwa na maoni yake, tena anayo haki ya kutoa ripoti moja kwa moja hata kwa Kamiti Kuu au Mwenye Kiti wa Kamiti Kuu bila ya kupitia kamiti inayomwongoza. Ni lazima iletwe hali ya kisiasa ya namna hiyo, yaani mbali ya uongozi pakuweko demokrasi, mbali ya nidhamu pakuweko uhuru, mbali ya nia ya pamoja pa-

kuweko furaha na uchangamfu wa kila mtu binafsi.

Maidara ya hatamu za kiserikali za udikteta wa tabaka la kifanya kazi, Jeshi la Ukombozi la Umma, na jumuia za umma za kimapinduzi zikiwemo Chama cha Vijana cha Kikoministi, jumuia za wafanya kazi, za wakulima masikini na wa kati wa daraja ya chini, za Walinzi Wekundu na nyinginezo, zote lazima zikubali kuongozwa na Chama.

Kifungu cha Sita: Idara ya uongozi ya daraja ya juu kabisa ya Chama ni Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Wajumbe na Kamiti Kuu ichaguliwayo nao. Maidara ya uongozi ya Chama ya kienyeji, ya kijeshi na sehemu mbali mbali ni mikutano mikuu ya wajumbe au mikutano ya wanachama katika daraja zile zile na kamiti za Chama zichaguliwazo nayo. Mikutano mikuu ya wajumbe wa Chama katika daraja

mbali mbali iitishwe na kamiti zake.

Kuitisha mikutano mikuu ya wajumbe wa Chama ya kienyeji na ya kijeshi, na wanachama waliochaguliwa wa kamiti za Chama, lazima kukubaliwa na oganezeshen za Chama za daraja za juu.

Kifungu cha Saba: Kwa kufuata kanuni ya kuwa na uongozi mmoja, mafungamano makubwa na umma na kurahisisha mambo, kamiti za Chama katika daraja mba-

li mbali zaweka maidara yake ya kazi au kutuma maidara yake ya kuziwakilisha.

MLANGO WA NNE

OGANEZESHEN KUU ZA CHAMA

Kifungu cha Nane: Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Wajumbe wa Chama huitishwa mara moja kila miaka 5. Katika hali maalum waweza kufanywa kabla ya wakati au kwa kuahirishwa.

Kifungu cha Tisa: Mkutano wa Wanakamiti Wote wa Kamiti Kuu ya Chama wachagua Ofisi ya Siasa ya Kamiti Kuu, Kamiti ya Kudumu ya Ofisi ya Siasa ya Kamiti Kuu, Mwenye Kiti na Makamu Mwenye Kiti wa Kamiti Kuu.

Mkutano wa Wanakamiti Wote wa Kamiti Kuu ya Chama waitishwa na Ofisi ya Siasa ya Kamiti Kuu.

Wakati wa kutokuweko Mkutano wa Wanakamiti

Wote wa Kamiti Kuu, Ofisi ya Siasa ya Kamiti Kuu na Kamiti yake ya Kudumu zatimiza madaraka na mamlaka ya Kamiti Kuu.

Chini ya uongozi wa Mwenye Kiti, Makamu Mwenye Kiti na Kamiti ya Kudumu ya Ofisi ya Siasa ya Kamiti Kuu, yawekwa maidara kadha yaliyo bora ya lazima, kwa uongozi mmoja kutanzua mambo ya kila siku kuhusu Chama, serikali na jeshi.

OGANEZESHEN ZA CHAMA ZA KIENYEJI NA ZA KIJESHI

Kifungu cha Kumi: Mikutano mikuu ya wajumbe ya Chama ya daraja ya wilaya na za juu yake au daraja ya rejimenti na za juu yake katika Jeshi la

Ukombozi la Umma hufanywa mara moja kila miaka 3. Katika hali maalum yaweza kufanywa kabla ya wakati au kwa kuahirishwa.

Kamiti za Chama za kienyeji na za kijeshi katika daraja mbali mbali zachagua kamiti zake za kudumu, makatibu na makamu makatibu.

MLANGO WA SITA

OGANEZESHEN ZA MSINGI ZA CHAMA

Kifungu cha Kumi na Moja

Moja: Kwa kawaida pawekwa matawi ya Chama katika viwanda, machimbo na mashirika, komune za umma, maidara ya serikali, mashule, maduka, mitaa, kampuni za Jeshi la Ukombozi la Umma

na idara nyinginezo za msingi; pakiweko wanachama wengi au mapigano ya kimapinduzi yakihitaji, pia yaweza kuwekwa matawi makuu au kamiti za msingi.

Kamiti za oganezeshen za msingi za Chama zafanyiwa uchaguzi kila mwaka mara moja. Katika hali maalum, zaweza kufanya uchaguzi kabla ya wakati au kwa kuahirishwa.

Kifungu cha Kumi na Mbili: Oganezeshen za msin-

gi za Chama zapaswa kunyanyua juu bendera kubwa nyekundu ya Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung, kuweka mbele siasa ya tabaka la kifanya kazi, kutukuza mtindo wa kuunganisha nadharia na matendo, mtindo wa kufanya mafungamano makubwa na umma na mtindo wa kutoa makosa na kujitoa makosa. Kazi zake muhimu ni kama zifuatazo:

1) Kuwaongoza wanachama na umma mkubwa wa ki-

mapinduzi katika kusoma na kutumia vitendoni Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung;

2) Siku zote kuwapa wanachama na umma mkubwa wa kimapinduzi mafundisho kuhusu mapigano ya kitabaka na ya misimamo miwili, na kuwaongoza katika kupambana kwa uthabiti na adui wa kitabaka;

3) Kufanya propaganda na kutimiliza kwa vitendo siasa za Chama, kutekeleza

maazimio ya Chama na kutimiliza kazi mbali mbali zinazopewa na Chama na taifa;

4) Kufanya mafungamano makubwa na umma, siku zote kusikiliza maoni na matakwa ya umma, kufanya mapigano ya kifikra yenye juhudi ndani ya Chama ili maisha ya Chama yawe yenye ujana na hamasa kubwa; na

5) Kuwaingiza wanachama wapya, kutekeleza ni-

dhamu ya Chama, mara kwa mara kuimarisha oganeze-shen za Chama, kutoa taka-taka na kuingiza kilicho kisafi, na kudumisha usafi wa kikosi cha Chama.

中国共产党章程

*

外文出版社出版（北京）
1969年（100开）第一版
編号：（斯）3050—2006
00022
3—Sa—1202Pk